Jarida la Wizara ya Afya

# Afya Habari

JARIDA LA MTANDAONI LA WIZARA YA AFYA | TOLEO, Na. 33, JULAI 2025






# TUNABORESHA AFYA

MTU NI AFYA, JALI AFYA YAKO




# YALIYOMO

SERIKALI YAJIZATITI KUDHIBITI HOMA YA INI ....Uk 2





SERIKALI YATAMBUA MCHANGO WA WATOA HUDUMA ZA AFYA KATIKA KUPIGANIA AFYA ZA WANANCHI.... Uk 3

VIWANDA VYA KUZALISHA VIFAA TIBA KUONGEZEKA NCHINI ...... Uk 4





WATANZANIA WAHIMIZWA KUWEKA JITIHADA ZA PAMOJA KUKABILIANA NA MAGONJWA YA MLIPUKOI.... Uk 5

MAZIWA YA MAMA NI KINGA DHIDI YA MAGONJWA KWA MTOTO...Uk 6





SERIKALI YAPOKEA VIFAA VYA SHILINGI MILIONI 569.7 KWA AJILI YA HUDUMA ZA SARATANI YA MATITI.... Uk 6

WANANCHI WA CHIKONJI WAPONGEZWA KWA UTHUBUTU ...... Uk 7



## BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Dkt. Seif Shekalaghe
KATIBU MKUU

**MHARIRI**
Roida N. Andusamile

**WAHARIRI WASAIDIZI**
Emmanuel Malegi
Atley Kuni

**WAJUMBE**
Said Makora
Hassan Kimweri
Shaban Juma
Cletus Sanga
Abdulwaheed Madenge
Aisha Swahibu
Anthony Ishengoma
Clement Robert
Mvuda Sufi

**WASANIFU**
Englibert Kayombo
Said Nyaoza

@wizara_Afyatz
www.moh.go.tz




# SERIKALI YAJIZATITI KUDHIBITI HOMA YA INI

**Na. Hassan Kimweri**
**RUVUMA**

Wananchi kote nchini wametakiwa kuchukua tahadhari dhidi ya homa ya ini ikiwa ni pamoja na kupata chanjo dhidi ya ugonjwa wa homa hiyo, huku akisisitiza kuwa, Serikali ya Tanzania imeweka nguvu kubwa kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa huo hatari.

Kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama Julai 28, 2025 alipokuwa akitoa tamko la Siku ya Homa ya Ini Duniani kwa wananchi kupitia vyombo vya habari mkoani Ruvuma.

"Serikali ya awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea na juhudi za utoaji wa huduma tiba na kinga dhidi ya Homa ya Ini, hivi sasa huduma za upimaji na matibabu zinatolewa kwenye Hospitali zote za Rufaa za Mikoa, Kanda na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili," alisema Waziri Mhagama.

Alibainisha kuwa vituo vya huduma za afya kuanzia ngazi ya Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati vitaendelea na utaratibu wa kupima Homa ya Ini na kutoa rufaa kwa huduma za Homa ya hiyo, huku mipango ya Serikali ikiendelea kuviwezesha vituo hivyo kutoa huduma kamili.

Waziri Mhagama alisema takwimu za utafiti wa UKIMWI ( THIS 2022/2023) zinaonyesha kuwa hali ya ushamiri wa Homa ya Ini ni asilimia 3.5, kwa Homa ya Ini inayosababishwa na virusi aina ya B na asilimia 0. kwa virusi vya homa ya ini inayosababishwa na aina ya virusi C ikiwa imeshuka kutoka takwimu za utafiti wa UKIMWI (THIS 2016/17) ilipokuwa asilimia 4. kwa homa ya Ini inayoambukizwa na virusi aina B na asilimia moja kwa Homa ya Ini inayoambukizwa virusi aina C.

Alibainisha kuwa kupungua kwa maambukizi ya Homa ya ini ni juhudi za pamoja kati ya Serikali na Wadau wa Sekta ya Afya walio kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa huo wakiwa na lengo la kidunia la kutokomeza ugonjwa huo ifikapo 2030.

"Hapa nchini Serikali inatoa huduma za chanjo ya Homa ya Ini aina ya B bila malipo yoyote kwa watoto wachanga na chanjo ya Homa ya Ini aina B kwa watu wazima inatolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa utaratibu wa kuchangia gharama kiasi," alisema Waziri Mhagama na kufafanua kuwa chanjo hiyo ilianza kutolewa kwa watoto nchini waliozaliwa kuanzia Mwaka 2002 kwani ni moja ya chanjo iliyopo kwenye mchanganyiko wa chanjo za magonjwa matano kwa chanjo moja (Pentavalent).

# SERIKALI YATAMBUA MCHANGO WA WATOA HUDUMA ZA AFYA KATIKA KUPIGANIA AFYA ZA WANANCHI

**Na. Abdulwaheed Madenge**
**DAR ES SALAAM**

Serikali imeendelea kutambua na kuthamini mchango wa watoa huduma na wahudumu wa Sekta ya afya kwa kuendelea kuwa kiungo muhimu katika kulinda na kupigania afya za Watanzania.

Hayo yalielezwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. Seif Shekalaghe, Julai 30, 2025, wakati wa ziara yake katika Taasisi ya Mifupa, Mishipa ya fahamu na Upasuaji wa Ubongo (MOI), jijini Dar es Salaam.

Akiwa katika ziara hiyo Dkt. Shekalaghe alituma salamu hizo kwa watumishi na watoa huduma na wataalam wa Sekta ya afya nchi nzima kutokana na namna wanavyojitoa kwa moyo, licha ya changamoto wanazokutana nazo katika kutekeleza majukumu yao.

“Utendaji kazi wenu ni mzuri sana na tunajivunia sana huko wizarani. Hongereni mno mnafanya kazi nzuri sana. Sisi kama Wizara tunathamini sana mchango wenu. Wananchi pia wanasifia ubora wa huduma mnazotoa,” alisema Dkt. Shekalaghe.

Aliongeza kuwa Serikali inatambua mchango wa kila mtoa huduma katika sekta ya afya, kuanzia ngazi ya msingi hadi taifa, na itaendelea kutoa motisha kadri itakavyoweza ili kuongeza ari na ufanisi katika utoaji wa huduma.

Aidha, aliwahimiza watumishi wa afya kuendelea kuwahudumia wananchi kwa haki, usawa, huruma na upendo, jambo ambalo litazidi kuimarisha uhusiano bora kati ya wahudumu na wananchi.

“Tuyafanyie kazi yale mapungufu madogo kabla hayajakua na kusababisha malalamiko kwa wananchi, Tujikite katika kuzizuia changamoto hizo kwa kusikiliza na kuzitatua kwa haraka na niwaombe muendelee kuwahudumia wananchi kwa haki, ili kuipa thamani kazi kubwa anayofanya Mhe. Rais kwa ajili ya sekta ya afya,” aliongeza Dkt. Shekalaghe.

"Kupitia mkataba huu wa huduma bora kwa mjeta, niwathibitishie Wizara ya Afya tumejipanga vizuri katika kuyatekeleza hayo kwa ubora unaotakiwa ili mwananchi anapoenda kupata huduma apate huduma iliyo bora na kwa wakati unaotakiwa," alisema Waziri Mhagama.






# VIWANDA VYA KUZALISHA VIFAA TIBA KUONGEZEKA NCHINI

**Na Hassan Kimweri**
**DODOMA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imetia saini ya makubaliano na kampuni ya kuzalisha vifaa vya maabara Abbott ya nchini Marekani yenye lengo la kujenga kiwanda kipya nchini kitakachoongeza upatikanaji wa vifaa tiba vitakavyosaidia kutambua magonjwa mbalimbali kwenye vituo vya afya.

Akizungumza katika utiaji saini wa makubaliano hayo Julai 12, 2025 Jijini Dodoma, Waziri wa afya Mhe. Jenista Mhagama amesema, kuongeza uzalishaji wa bidhaa tiba ndani ya nchi ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali ili kupunguza gharama za utegemezi wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

Alisema, kuanzisha kiwanda cha uzalishaji wa vifaa tiba nchini kutafanya Tanzania kuwa kituo cha umahiri kwenye tiba, kupunguza utegemezi wa kuagiza nje kwa asilimia 20 na kurahisisha upimaji wa magonjwa kama Virusi Vya Ukimwi, Kaswende na homa ya Ini.

“Sasa tunapokwenda ni kuzuri zaidi na niliwaambia tuna vipaumbele 10, kimojawapo ni kuongeza uzalishaji wa bidhaa tiba ndani ya nchi na kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi, tunashukuru sana kwa uwekezaji uliofanywa tumeweza kupunguza utegemezi kutoka asilimia 100 mpaka asilimia 80,” alisema Waziri Mhagama.

Aidha, Waziri Mhagama alisema dhima ya Serikali ya awamu ya sita ni kuwekeza fedha nyingi kwenye Wizara ya Afya kwa lengo la kuongeza huduma zenye tija kwa wananchi ikiwemo matumizi ya teknolojia na mifumo ya akili mnemba itakayorahisiha utolewaji wa tiba kwa wananchi.

Kwa upande wake Makamu wa Rais wa Uendeshaji Kibiashara, Idara ya Magonjwa ya Kuambukiza kutoka kampuni ya Abbott, Bw. Steven Henn alisema makubaliano hayo yaliyoanza mwezi Oktoba 2024, yamekuja yakiwa na nia ya dhati ya kuboresha huduma za afya kati ya Serikali ya Tanzania na kampuni ya Abbott.

"Kupata nafasi hii ya kuweka rasmi makubaliano haya yatakayokuwa ya muhimu kati ya Abbot na Wizara ya Afya kutufikisha kwenye hatua kubwa ya uwajibikaji wenye lengo la kuboresha huduma za afya," alisema Bw. Henn.

Naye, Mfamasia Mkuu wa Serikali Bw. Daudi Msasi alisema makubaliano hayo yana nia ya kuleta mabadiliko ikiwemo kupunguza gharama zilizokuwa zikitumika na Serikali kuagiza vifaa tiba nje ya nchi vilivyogharimu zaidi ya Shilingi Bilioni 51 kila mwaka.

# WATANZANIA WAHIMIZWA KUWEKA JITIHADA ZA PAMOJA KUKABILIANA NA MAGONJWA YA MLIPUKO

**Na Aisha Swahibu**
**ARUSHA**

Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Grace Magembe ametoa wito kwa Watanzania kuweka jitihada za pamoja katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko.

Dkt. Magembe alibainisha hayo Julai 24, 2025 Jijini Arusha katika Kikao cha sekta mbalimbali Bara na Visiwani cha usimamizi wa Mradi wa Mfuko wa Pandemic unaosaidia kujiandaa kukabiliana na Magonjwa ya mlipuko(Pandemic Fund) kilichoratibiwa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani(WHO).

Dkt.Magembe alisema ni muhimu kwa kila mmoja kuweka jitihada katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko kwa kuzingatia kanuni za afya ikiwemo kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni.

“Ujumbe wangu kwa Watanzania ni lazima wachukue tahadhari, magonjwa mengi ya mlipuko yanazuilika endapo utachukua tahadhari, kipindupindu kinazuilika endapo utazingatia kanuni za afya , matumizi ya vyoo, kuepuka kujisaidia ovyo,kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni lakini magonjwa kama Mpox yanazuilika kwa kuepuka misongamano na kugusana na mtu aliyeonesha dalili za ugonjwa huo.

Akizungumzia kuhusu mfuko wa Pandemic Fund Dkt. Magembe alisema Mfuko huo umekuwa na mchango mkubwa katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko.

“Serikali kwa kushirikiana na Wadau tuliomba fedha kupitia mradi wa “Pandemic Fund kwa ajili ya kusaidia nchi yetu iweze kujiandaa kukabiliana na majanga yanapotokea na kuimarisha mifumo ya afya,tunashukuru uongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanikisha mradi huu kuja Tanzania ambao utatekelezwa Tanzania Bara pamoja na Zanzibar kwani utatuwezesha kuandaa wataalamu wetu, mifumo ya kugundua magonjwa kabla hayajatokea na maabara zetu na uratibu wa pamoja chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu”alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, Bw. Makame Khatib Makame alisema Mradi wa Pandemic Fund utaleta tija kubwa katika uratibu wa pamoja katika utekelezaji wa dhana ya afya moja hasa tahadhari za pamoja.



# MAZIWA YA MAMA NI KINGA DHIDI YA MAGONJWA KWA MTOTO




**Na Clement Robert**
**DAR ES SALAAM**

Jamii imeaswa kuzingatia afya za watoto wachanga kwa kutoa nafasi ya mapumziko kwa wanawake waliopo katika sekta rasmi na isiyo rasmi ili waweze kuwanyonyesha kikamilifu watoto wao kwa kutumia maziwa ya mama kama inavyopendekezwa na wataalam wa afya.

Hayo yalibainishwa Julai 30, 2025, jijini Dar es Salaam na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Afya), Prof. Tumaini Nagu, wakati wa akifungua maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji wa Maziwa ya Mama Duniani pamoja na uzinduzi wa Mwongozo wa Kitaifa wa Kuzuia na Kutibu Ukondefu na Uvimbe unaotokana na Ukondefu kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano jijini Dar es Salaam.

Prof. Nagu alisema kuwa, kwa kuzingatia taratibu zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO), watoto wanapaswa kupewa uangalizi wa karibu na kunyonya maziwa ya mama ipasavyo ili kuboresha afya na kuwakinga dhidi ya magonjwa yatokanayo na ukosefu wa virutubisho muhimu vilivyomo kwenye maziwa ya mama.

“Miongozo inatuelekeza kwamba mtoto anatakiwa aanze kunyonya maziwa ya mama ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa, aanze kula vyakula vingine akifikishapo miezi sita, lakini bado aendelee kunyonya hadi atakapofikisha miaka miwili, kwa sababu maziwa ya mama yana virutubisho vyote muhimu na hutoa kinga dhidi ya magonjwa,” alisema Prof. Nagu.

Naye Mkurugenzi wa Shirika la Action Against Hunger Tanzania, Bw. Zacharia Imeje, alisema uzinduzi wa mwongozo huo utawasaidia wahudumu wa afya, ambao ndio watu wa karibu na watoto, kushughulikia changamoto za lishe duni na ukondefu kwa ufanisi zaidi.

“Sisi kama taifa tunaweza kushughulikia mahitaji ya lishe kwa watoto wetu kwa njia bora. licha ya muda uliotumika kuukamilisha mwongozo huu, tuna furaha kwamba sasa umeidhinishwa na Wizara ya Afya. Tunatarajia wadau wote wanaoshughulika na utapiamlo watautumia kwa manufaa mapana ya afya za watoto wa Kitanzania,” alisema Bw. Imeje.

Takwimu zinaonesha kuwa viwango vya unyonyeshaji wa watoto nchini Tanzania vinaendelea kuimarika kwani Idadi ya watoto wanaonyonyeshwa maziwa ya mama pekee imeongezeka kutoka asilimia 58 mwaka 2018 hadi asilimia 64 mwaka 2022.

Aidha watoto wanaonyonyeshwa ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa wameongezeka kutoka asilimia 53.5 mwaka 2018 hadi asilimia 70 mwaka 2022, huku watoto wanaoendelea kunyonya hadi umri wa miaka miwili au zaidi wakiwa ni asilimia 62.



# SERIKALI YAONGEZA MASHINE MPYA TATU ZA TIBA MIONZI

**Na Abdulwaheed Madenge**
**DAR ES SALAAM**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. Seif Shekalaghe, amesema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan imenunua mashine mpya tatu za tiba mionzi kwa ajili ya kuboresha huduma za matibabu ya saratani nchini.

Dkt. Shekalaghe alisema hayo Julai 29, 2025 wakati wa ziara yake katika Taasisi ya Saratani Ocean Road, ambapo alieleza kuwa hatua hiyo ni sehemu ya jitihada za Serikali katika kutatua changamoto ya muda mrefu ya ucheleweshwaji wa huduma kwa wagonjwa kutokana na uhaba wa mashine hizo.

"Rais wenu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ndiye aliyetoa fedha kwa ajili ya mashine hizi baada ya kusikia kilio cha wananchi kuhusu ucheleweshwaji wa huduma za mionzi kutokana na uhaba wa vifaa," alisema Dkt. Shekalaghe.

Aidha, alitumia nafasi hiyo kuwaomba wananchi kuwa wavumilivu wakati mashine hizo zikiendelea kufungwa na kuanza kutumika rasmi, huku akiwasihi kuendelea kushirikiana na watumishi wa afya.

Katika hatua nyingine, Dkt. Shekalaghe aliwapongeza watumishi wa sekta ya afya kwa kujituma na kutoa huduma kwa weledi mkubwa licha ya changamoto mbalimbali zinazowakabili.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dkt. Diwani Msemo, alitoa shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwezesha upatikanaji wa mashine hizo za uchunguzi na matibabu katika taasisi hiyo, akisema kuwa hatua hiyo itaongeza kasi na ufanisi katika kuhudumia wagonjwa wa saratani.

# WANANCHI WA CHIKONJI WAPONGEZWA KWA UTHUBUTU

**Na Isha Swahibu**
**LINDI**

Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imewapongeza wananchi na uongozi wa Kijiji cha Chikonji kilichopo mkoani Lindi kwa juhudi zao za kujitolea kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuboresha huduma za afya, hususan kwa kuanzisha ujenzi wa jengo la wodi ya uzazi kwa ajili ya akinamama na watoto.

Pongezi hizo zilitolewa Julai 24, 2025 na Bi. Faraja Mgeni, Afisa kutoka Idara ya Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto , Wizara ya Afya, wakati wa ziara ya ufuatiliaji na usimamizi shirikishi wa utekelezaji wa Mradi wa Ukarabati wa Vituo vya Afya unaofadhiliwa na Taasisi ya Susan Thompson Buffett Foundation (STBF). Mradi huo unalenga kuboresha huduma za afya ya uzazi kwa akinamama na watoto wachanga.

Bi. Faraja alieleza kuwa wananchi wa Chikonji walichangisha Shilingi Milioni 4 kwa ajili ya kuanzisha ujenzi wa wodi hiyo kutokana na changamoto walizokuwa wakikabiliana nazo ambapo pia Halmashauri nayo ilichangia Shilingi Milioni 4, hivyo kuwezesha kuanza kwa ujenzi huo.

"Wananchi walijichangisha Shilingi Milioni 4, na Halmashauri ikatoa Milioni 4 nyingine jumla ikawa Milioni 8 ndizo fedha zilizoanzisha ujenzi huu, sasa fedha kutoka STBF zitasaidia kumalizia ujenzi huu ulipoishia," alisema Bi. Faraja.

Aidha, Bi. Faraja alibainisha kuwa ufuatiliaji unaofanywa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI unalenga kuangalia hatua zilizofikiwa katika ngazi ya mkoa, halmashauri na vituo vya afya vilivyopokea fedha, pamoja na kutoa maelekezo ya namna ya kufanikisha utekelezaji wa miradi hiyo.

Kwa upande wake, Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Lindi Mjini ambaye pia ni Afisa Miradi wa wilaya hiyo, Dkt. Charity Ngezi, alisema kuwa Kituo cha Afya cha Chikonji kilishapokea fedha kwa ajili ya ukarabati na kwamba ukarabati huo utakamilika kwa wakati.

"Tulifanya kikao na wananchi mara baada ya kupokea fedha hizo na kuwaeleza kuhusu mradi utakaoanza. Wananchi walifurahia sana na kuona kwamba changamoto ya huduma za uzazi kwa akinamama imepata ufumbuzi," alisema Dkt. Ngezi





# SERIKALI, WADAU WAKUTANA KUJADILI UIMARISHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

**Na Mvuda Sufi**
**DODOMA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais TÀMISEMI, wamekutana na wadau kutoka Shirika la Kimataifa la masuala ya Afya la Korea (Korea Foundation for International Healthcare-KOFIH) kujadili mikakati ya pamoja itakayowezesha taasisi hiyo kuendelea kutoa ufadhili ili kuimarisha sekta ya afya nchini.

Akifungua warsha hiyo Julai 24, 2025 jijini Dodoma, kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Mkurugenzi wa Sera na Mipango kutoka Wizara ya Afya Bw. Amour Amour alisema warsha hiyo inadhihirisha wazi ni jinsi gani taasisi ya KOFIH iko tayari kushirikiana na Serikali kwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya.

"Tumekutana hapa tukiwa na maono ya pamoja ya kuhakikisha kuwa mifumo ya sekta ya afya inaimarishwa ikiwa ni pamoja na rasilimali watu miundombinu na ubunifu," alifafanua Bw. Amour.

Alisema kuwa Tanzania iko kwenye hatua za mabadiliko katika sekta ya afya hivyo kama nchi haiwezi kufanya mabadiliko haya bila kuwa na ushirikiano na wadau kama KOFIH ambao wamekuwa ni msaada mkubwa katika kuimarisha huduma za afya nchini.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa KOFIH Bw. Gyeongbae Seo alisema taasisi yake inaahidi kuendelea kuimarisha sekta ya afya nchini ikiwa ni pamoja na kugharamia mafunzo kwa wataalam wa afya na kuboresha miundombinu ya sekta ya afya utakaowezesha utoaji wa huduma bora za afya.

Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa katika warsha hiyo ni pamoja kuimarisha mifumo ya afya kupitia ushirikiano wa kimkakati, kuwekeza katika rasilimali watu, miundombinu na ubunifu.

# WATAKIWA KUWALEA WATOTO KWA KUZINGATIA USHAURI, MAELEKEZO YA WATAALAM




**Na Abdulwaheed Madenge**
**ARUSHA**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. Seif Shekalaghe, ametoa wito kwa wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kuzingatia ushauri na maelekezo ya wataalam wa afya na malezi ili kuwalea watoto, kwa kuweka mkazo maalum wa lishe bora, malezi yenye upendo na mazingira salama kwa ajili ya ustawi wao, kwakuwa watoto ni hazina ya taifa la kesho.

Dkt. Shekalaghe alitoa wito huo Julai 23, 2025, mkoani Arusha, wakati akifungua Kongamano la pili la Kitaifa la Afya na Ustawi wa Watoto, ambapo amesisitiza kuwa taifa haliwezi kuwa na viongozi bora wa baadaye ikiwa jamii haitawalea watoto kwenye misingi imara ya afya, elimu na maadili.

“Watoto wasipopata malezi vizuri, wakakosa lishe bora, mazingira salama na malezi yanayojali maendeleo yao ya kimwili na kiakili, hatuwezi kuwa na viongozi bora wa kesho, rai yangu ni muhimu jamii kutambua na malezi bora hujengwa kwa kuzingatia ushauri wa wataalam wa afya na wataalam wa malezi,” alisema Dkt. Shekalaghe.

Aliongeza kuwa familia zinapaswa kuzingatia kila nyanja ya afya ya mtoto kuanzia mlo anaopata, mazungumzo ya kila siku, michezo anayoshiriki, hadi mazingira anayoishi.

“Afya siyo tu kukosekana kwa ugonjwa, bali ni hali njema kimwili, kiakili, kijamii na kiutamaduni. Tunapaswa kuwalea watoto wetu kwa njia sahihi ili wajenge taifa lenye msingi thabiti,” alisisitiza.

Dkt. Shekalaghe pia aliwahimiza wataalam na watoa huduma za afya nchini, hususan wale wanaohudumia watoto, kulenga zaidi kuzuia vifo na kujikita pia kwenye kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa lishe bora na malezi chanya kwa watoto.

Alisema ushirikiano huo ni muhimu katika kufanikisha juhudi za kudhibiti na kuzuia magonjwa yanayoweza kutokomezwa kwa njia ya chanjo.



# SERIKALI YATOA BILIONI 298 KUGHARAMIA MATIBABU YA KIFUA KIKUU, UKIMWI, MALARIA NCHINI

**Na Clement Robert**
**DODOMA**

Serikali ya Tanzania kwa kipindi cha mwaka 2024/25 na 2025/26 imetoa jumla ya Dola Milioni 114 sawa na Shilingi Bilioni 298 za kitanzania kuongeza manunuzi ya dawa na vifaa tiba ili kufidia fedha zilizokuwa zikitumika kupambana na magonjwa ya Kifua Kikuu, UKIMWI na malaria nchini.

Hayo yalielezwa na Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Grace Magembe, Julai 21, 2025 mkoani Dodoma wakati wa kikao kazi cha kupitia bajeti ya Mfuko wa Dunia (Global Fund) ambapo Serikali imefikia hatua hiyo ili kwenda sambamba na mahitaji ya watanzania kufuatia baadhi ya nchi kupunguza ufadhili wake.

"Mtakumbuka hivi karibuni kuna fedha ambazo baadhi ya nchi wahisani zimepunguza ufadhili wake katika kuhudumia magonjwa ya kifua kikuu, UKIMWI na malaria ili kupambana na magonjwa hayo nchini, hata hivyo Serikali kwa uharaka imetoa Dola za Kimarekani Milioni 54 sawa na Shilingi Bilioni 140 za kitanzania kwa mwaka wa fedha 2024/25," alisema Dkt. Magembe.

Aliongeza kuwa katika mwaka wa fedha 2025/26 Serikali iliongeza fedha hizo ili kukidhi mahitaji zaidi ya mwananchi wa chini ambao wamekuwa wakisumbuliwa na magonjwa hayo.

"Mwaka huu wa fedha wa 2025/26 Serikali pia imeongeza Dola Millioni 60 sawa na Shilingi Bilioni 159 za kitanzania kwa ajili ya magonjwa kufidia hayo mapungufu ya fedha ambayo yametoka kwa nchi wahisani, lengo kuu la haya yote ni kuhakikisha tunaboresha ubora wa huduma kwa wananchi na wahitaji kutoka maeneo mbalimbali," alisema Dkt. Magembe

Kikao kimekutanisha wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi wakiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu, OR-Tamisemi, Wizara ya Fedha na Wizara ya Afya, Ubalozi wa Marekani pamoja na washirika kutoka Shirika la Afya Ulimwenguni, TNCM na LFA huku lengo kuu likiwa ni kujadili namna ya matumizi ya rasilimali zinazopatikana kuendana na mahitaji ya jamii.

# UIMARISHAJI UBORA WA AFYA, USTAWI WA WATOTO NI NYENZO MUHIMU KUIMARISHA AFYA ZA WATOTO NA VIJANA - DKT. SHEAKALAGHE

**Na Abdulwaheed Madenge**
**ARUSHA**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. Seif Shekalaghe amesema Mpango wa Kuimarisha Ubora wa Afya na Ustawi wa Watoto ni nyenzo muhimu katika kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa watoto na vijana nchini.

Dkt. Shekalaghe alisema hayo Julai 23, 2025 Mkoani Arusha wakati wa kongamano la Pili la Kitaifa la Afya na Ustawi wa Watoto baada ya kuzindua rasmi mpango huo wenye lengo la kushughulikia changamoto zinazowakabili watoto na vijana ikiwemo matatizo ya lishe, mimba za utotoni na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Mpango huo umeandaliwa na Chama cha Madaktari Bingwa wa Watoto Tanzania (Pediatric Association of Tanzania – PAT) kwa kipindi cha miaka Mitano (5) kuanzia mwaka 2025 hadi 2030 ambao umejikita katika kushughulikia vikwazo vinavyokwamisha maende ya kiafya kwa watoto na vijana, hasa wenye umri wa miaka 15-19.

Vipaumbele vya mpango huo ni pamoja na Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Wizara ya Afya na wadau wa sekta ya afya,Kushawishi na kuandaa sera zitakazosaidia kuimarisha afya na ustawi wa watoto,Kuwekeza katika tafiti na ubunifu wa kitabibu ili kuboresha huduma,Kutoa mafunzo endelevu kwa Madaktari Bingwa na watumishi wengine wa afya,

Pia mpango huo unalenga kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali, Sekta Binafsi pamoja na mashirika ya Kimataifa katika kukuza na kuimarisha rasilimali zitakazowezesha utekelezaji wa huduma bora kwa watoto na vijana.

Awali, akizungumza katika uzinduzi huo, rais Mteule wa Chama cha Madaktari Bingwa wa Watoto Tanzania Dkt. Alex Mphuru, aliiomba Serikali pamoja na wadau wa maendeleo kushirikiana katika utekelezaji wa mpango huo ambao unakadiriwa kugharimu jumla ya Shilingi Bilioni 2.2.

"Kwa ujumla mpango huu ni hatua muhimu katika kuelekea kujenga kizazi chenye afya njema, lishe bora, na ustawi wa kudumu kwa watoto na vijana nchini Tanzania," alisema Dkt. Mphuru



# WELEDI, UMAKINI WATAKIWA WAKATI WA UCHUKUAJI WA SAMPULI ZA MAJI - MWAKITALIMA




**Na Clement Robert**
**MOROGORO**

Wataalam wa afya ya mazingira kutoka halmashauri mbalimbali nchini wametakiwa kuzingatia weledi na mafunzo waliopatiwa wakati wa uchukuaji wa sampuli za maji kwa ajili ya vipimo, ili kubaini usalama wa maji ya kunywa na kuzuia magonjwa ya mlipuko.

Hayo yalibainishwa na Julai 17, 2025 mkoani Morogoro na Mkuu wa Sehemu ya Chakula Salama, Maji Salama na Usafi wa Mazingira kutoka Wizara ya Afya, Bw. Anyitike Mwakitalima, wakati wa mafunzo ya vitendo kuhusu usalama wa maji ya kunywa.

“Wataalamu hakikisheni mnatumia kwa usahihi kila hatua mliyojifunza kabla ya kwenda kuchukua sampuli kwenye maeneo husika na kupata matokeo sahihi, yanayokubalika kitaalamu kwa hatma ya afya za watanzania," alisema Bw. Mwakitalima

Naye, Afisa afya Mwandamizi mtaalam wa Epidemologia Bw. Ambakisye Mchiche alibainisha kuwa kufanya kwa vitendo kunatoa wepesi wa kuelewa mafunzo hayo na kutimiza dhima yake ya kuhakikisha usalama wa maji ya kunywa kwa wananchi unakuwa mkubwa

Alisema sampuli zilizochukuliwa kutoka mfereji, mito, visima virefu, visima vifupi na maji ya bomba ni kwa lengo la kuweka uhakiki na kutofautisha matokeo ili iwe rahisi kwa wataalam wanaopata mafunzo kuona tofauti baina ya maji yaliyo salama na ambayo hayafai kwa matumizi ya kunywa

"Utekelezaji wa mafunzo kwa njia ya vitendo hurahisisha uelewa wa dhana nzima, sambamba na kutimiza lengo la kuhakikisha maji ya kunywa kwa wananchi yanakuwa salama," alisema Bw. Mchiche

Mafunzo ya vitendo kwa uchukuaji na upimaji wa sampuli za maji yameonesha dhamira ya Serikali ya kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anapata huduma bora ya maji salama, huku wataalam wakiwekwa mstari wa mbele ili kulinda afya ya jamii kwa kupewa elimu kuhusu mbinu bora za uchunguzi wa maji, viashiria vya uchafuzi, na matumizi ya vifaa vya kisasa vya kupima ubora wa maji, kama sehemu ya afua ya kitaifa wa kupambana na magonjwa yanayotokana na maji machafu.




# SERIKALI YAAHIDI KUONGEZA WIGO WA UTOAJI HUDUMA ZA AFYA

**Na Mvuda Sufi**
**DODOMA**

Naibu Waziri ofisi ya Rais TAMISEMI anayeshughulikia masuala ya Afya Dkt. Festo Dugange, amesema Serikali itaendelea kuongeza wigo wa utoaji na upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi huku akiwasisitiza watoa huduma za afya kuwa wabunifu na kuendelea kuwajibika kwa wananchi.

Dkt. Dugange alisema hayo Julai 13, 2025 wakati akikufunga Mkutano Mkuu wa Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri uliofanyika jijini Dodoma katika ukumbi wa mikutano wa wa Jakaya Kikwete.

Dkt. Dugange alisema kwa mwaka wa fedha 2025/26 Serikali itajenga hospitali 43 za halmashauri, pia itanunua vifaa tiba kwajili ya hospitali 142 sambamba na kujenga zahanati 184.

"Kupitia vyanzo vya ndani vya Halmashauri, Serikali imepanga kutekeleza miradi mbali mbali ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya 28, ukamilishaji wa vituo vya afya 74 pamoja na ujenzi wa zahanati 32 pamoja na ukamilishaji wa zahanati 325," alisema Dkt. Dugange.

Katika hatua nyingine Dkt. Dugange alisema ni muhimu kuwa na sanduku la maoni ili kupata mrejesho na changamoto za wananchi ili zipatiwe ufumbuzi.

"Nawaagiza waganga wakuu wa halmshauri na mikoa kuendelea kusikiliza kero za wananchi kuhusiana na Afya pia kwenye kila kituo cha Afya au Zahanati ni lazima kuwe na sanduku la maoni, " alisema Dkt. Dugange.

Akihitimisha Mkutano huo, Dkt. Dugange aliwataka watumishi wa Afya kuendelea kuwa wabunifu ili kukidhi mahitaji ya wananchi pamoja na kuzingatia maadili ya kazi yao.

Wizara ya Afya kwa ushirikiano na Ofisi ya Rais TAMISEMI iliandaa Mkutano wa siku kwa ajili ya Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri kujadiliana na kuweka mikakati ya kuboresha sekta ya afya nchini na utoaji huduma kwa muda wa siku mbili.



# WATANZANIA WAHIMIZWA KUZIPA KIPAUMBELE HOSPITALI ZA NDANI KWA HUDUMA ZA VIPIMO

**Na Hassan Kimweri**
**MTWARA**

Watanzania wameaswa kuzipa kipaumbele hospitali za ndani ya nchi kwa kufanya uchunguzi wa afya wa awali kwa kuwa Serikali chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imewekeza zaidi katika Sekta ya Afya na zina uwezo wa kufanya uchunguzi huo hapa nchini.

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama alisema hayo Julai 10, 2025 alipofanya ziara katika Hospitali ya Benjamini Mkapa (BMH) pamoja na kukagua Mradi wa Ujenzi wa Jengo la 'Radio Therapy', Kuzindua Kliniki ya tiba utalii na kushuhudia utiaji saini wa hati ya makubaliano ya ushirikiano kati ya BMH, JKCI na KCMC.

"Tumezoea kufanya uchunguzi wa afya nje ya nchi tukiamini uchunguzi ukifanywa nje ndio unakuwa na majibu sahihi, kwa uwekezaji uliofanyika hapa Benjamini Mkapa, Muhimbili, MOI, Mloganzila na taasisi zetu nyingine uwezo wa kufanya uchunguzi wa awali kwa sasa ni mkubwa na tunao," alisema Waziri Mhagama.

Aidha, Waziri Mhagama alisema uanzishaji wa kliniki ya tiba utalii katika hospitali hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020, hivyo amewataka Wenyeviti wa Bodi na Wakurugenzi kuzingatia maelekezo ya Serikali ili kuhakikisha huduma bora zinawafikia Watanzania na wageni wengi watakaokuja nchini.

"Lakini wito wangu mwingine ni kwamba, vituo vyote vya kutolea huduma za afya kwenye ngazi ya Kanda, Taasisi zinazotoa huduma za afya, Hospitali za Kanda, naomba tuanzishe huduma hii kama iliyoanzishwa na Hospitali ya Benjamini Mkapa kwa wale ambao hawana," alisema Waziri Mhagama.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Hospitali ya Benjamini Mkapa Prof. Edward Hosea alisema kwa niaba ya bodi yake wamepokea maelekezo yote aliyoyatoa Mhe. Waziri Mhagama ikiwemo ya usimamizi wa mradi wa ujenzi wa jengo la Radiotherapy linalotakiwa kukamilika hadi ifikapo mwezi Disemba 2025.

Naye, Prof Abel Nkono Makubi, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa alisema kwa sasa hospitali hiyo inatoa huduma za kibigwa 20 na kibobezi 17 ambapo pia inapokea wagonjwa zaidi ya 1,200 kwa siku.

"Lakini pia katika hospitali yetu tunatoa huduma za upasuaji kwa njia ya matundu, kupandikiza uloto, upasuaji wa ubongo, mfumo wa mkojo pamoja na macho kwa kutumia tekinolojia ya kisasa," alisema Prof. Makubi.

# WHO YAKABIDHI VIFAA VYA SHILINGI MILIONI 112 KUDHIBITI MAGONJWA YA MILIPUKO KAGERA

**Na Roida Andusamile**
**KAGERA**

Shirika la Afya Duniani (WHO) limekabidhi vifaa vya afya vyenye thamani ya Shilingi Milioni 112 ili kuimarisha tiba ya magonjwa ya mlipuko katika wilaya za Biharamulo na Muleba mkoani Kagera.

WHO ilikabidhi vifaa hivyo kupitia Wizara ya Afya ikiwa ni muendelezo wa kupambana na magonjwa ya mlipuko ambayo yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara hususani mlipuko wa ugonjwa wa Murburg ambao hivi karibuni ulijitokeza katika mkoa huo.

Kaimu Mkurugenzi wa Dharura na Maafa kutoka Wizara ya Afya Dkt. Erasto Sylvanus alipokea vifaa hivyo Julai 15, 2025 kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Grace Magembe.

Dkt. Silvanus alivitaja vifaa hivyo kuwa ni vitanda vya kisasa vya kulaza wagonjwa, machine za kufulia mashuka,stendi za kuwekea dawa, ndoo za kuhifadhi maji na kufanyia usafi katika vituo vya afya pamoja na vifaa vya kufanya uchunguzi wa kina.

Kiongozi huyo wa Wizara aliongeza kuwa, vifaa vilivyopokelewa ni jitihada zinazoendelea kufanyika katika kurejesha hali nzuri ya kupambana na magonjwa ya mlipuko yanapotokea huku akiwataka watumiaji wa vifaa hivyo kuvitunza ili viweze kukaa kwa muda mrefu ili kuwasaidia wananchi.

"Ugonjwa huu umetupa mafunzo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kutoa taarifa ya dharura pale wanapoona ugonjwa usio wa kawaida, kuimarisha utayari, kushirikisha jamii pamoja na kuunganisha wadau katika kuudhibiti,"alisema Dkt. Silvanus.

Naye Mwakilishi Mkazi wa WHO Dkt. Galberth Fadjo alisema kuwa shirika hilo kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wameweka jitihada kubwa na kuchukua hatua za haraka ya kudhibiti magonjwa yenye nguvu kama Murbug yasisambae zaidi na kuhakikisha wanaopata ugonjwa wanarudi katika hali ya kawaida haraka bila kuleta madhara.

Alisisitiza kuwa, mlipuko wa ugonjwa wa Marburg katika mkoa wa Kagera uliotokea Wilaya ya Bukoba mwaka 2023 na Wilaya ya Biharamulo mwaka 2025, Serikali ilipambana kuthibiti ugonjwa huo bila kuathiri shughuli nyingine na kurejesha hali ya kawaida katika jamii huku akisema kuwa huo ni mfano wa kuigwa kwa nchi nyingine zinazokabiliana na majanga.

Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera Bw. Steven Ndaki aliishukuru WHO pamoja na Wizara ya Afya kwa kuona umuhimu wa kupeleka vifaa hivyo vyenye thamani kubwa kwakuwa vitasaidia kuokoa maisha ya wananchi huku akitoa wito kwa wataalam kuvitunza vifaa hivyo kama walivyoelekezwa.



# WATAKIWA KUKAMILISHA MAPEMA MKAKATI WA ELIMU YA AFYA KWA UMMA

**Na Clement Robert**
**DAR ES SALAAM**

Wajumbe wa Kikosi kazi kinachoandaa Mpango Mkakati wa Elimu ya Afya kwa Umma wametakiwa kukamilisha mapema mchakato wa rasimu ya mpango mkakati huo ili kutoa nafasi ya hatua nyingine muhimu za kuidhinishwa na kuanza kutekeleza.

Rai hiyo ilitolewa Julai 15, 2025 na Mkurugenzi Msaidizi wa Sehemu ya Elimu ya Afya kwa Umma Dkt. Ona Machangu kupitia kikao kazi kinachofanyika jijini Dar es Salaam, akikiagiza kuongeza kasi ya utendaji na kukamilisha haraka ili hatua nyingine za kuhalalisha rasimu hiyo zifuate haraka iwezekanavyo.

Alisema, kuongezeka kwa wadau mbalimbali ni ishara ya wazi ya kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Afya kupitia Sehemu ya Elimu ya Afya kwa Umma, hivyo rasimu hiyo ikikamilika kwa haraka itaongeza ubora na thamani ya mambo yanavyofanyika.

"Natamani baada ya kikao hiki rasimu iende hatua zinazofuata, ni hatari kuendelea kutekeleza afua za elimu ya afya kama hauna mikakati, sababu hili ni miongoni mwa mambo yaliyowekewa mkazo kwenye - marejereo ya Mpango Mikakati ya Sekta ya Afya," alieleza Dkt. Machangu.

Aidha, rasimu hiyo itakapokamilika italeta mapinduzi katika utoaji wa elimu ya afya kwa kutumia teknolojia ya kisasa na mifumo ya kidijitali kwa lengo la kuweka msingi wa kuboresha ubora, ufanisi, usambazaji, na upatikanaji wa huduma za elimu ya afya kwa jamii nchini.

Katika taarifa yake ya kikao kazi cha kuadhimisha rasimu ya mpango mkakati wa elimu ya afya kwa umma, Wizara inalenga kuhakikisha kuwa afua za elimu ya afya zinatolewa kwa kutumia ushahidi wa kisayansi, takwimu sahihi, na mbinu bora za kitaalamu.

Katika kuhakikisha utekelezaji wake, Wizara kupitia Sehemu ya Elimu ya Afya kwa Umma imetengeneza zana za ukusanyaji na utoaji taarifa za afya ambazo ni sanifu na rahisi kutumia, Tafiti za ubunifu na utafiti shirikishi kwenye jamii zinatumika kuunda afua zinazojibu mahitaji ya kijamii na timu za elimu ya afya kupewa vifaa vya kidijitali, na programu za kudhibiti takwimu kwa ufanisi.





# VIONGOZI WA DINI WATAKIWA KUWA MABALOZI KWA JAMII KUJIKINGA NA MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA

**Na Aisha Swahibu**
**DODOMA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imetoa wito wa viongozi wa dini nchini kuwa mabalozi kwa jamii katika kutoa elimu ya namna bora ya kubadilisha mtindo wa maisha hususani kwenye lishe na kujenga taratibu za kupima afya zao mara kwa mara ili kujikinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza.

Hayo yalibainishwa Julai 10, 2025 Jijini Dodoma na Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Kinga Dkt. Otilia Gowelle, wakati akifungua kikao kazi cha viongozi wa dini kuhusu elimu ya Kinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza.

Dkt. Gowelle alisema magonjwa yasiyoambukiza ni changamoto kubwa, lakini pia changamoto hiyo inaweza kushughulikiwa kupitia elimu, ushirikiano na mabadiliko ya mitindo ya maisha.

“Viongozi wa dini na wanajamii kwa ujumla mnalo jukumu muhimu la kusaidia kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa afya bora ikiwa ni pamoja na kuchukua tahadhali mapema ili kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza na changamoto zinazosababisha afya ya akili,” alisema Dkt. Gowelle.

Alieleza kuwa kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Afya, takribani asilimia 33 ya vifo vyote vinavyotokea nchini kila mwaka, husababishwa na magonjwa yasiyoambukiza, ni sawa na mtu mmoja (1) kati ya watatu (3) hufariki kutokana na maradhi hayo, jambo linaloathiri nguvu kazi ya taifa na kuongeza gharama za matibabu kwa familia na Serikali.

Naye Kaimu Mkurugenzi Idara ya Tiba Dkt. Winfred Kilima aliwataka viongozi wa dini na waandishi wa habari kutumia nguvu ya ushawishi waliyonayo kubadili mitazamo ya jamii na namna bora ya kujikinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza ili yasifike kwenye ngazi ya tiba.

“Tunatamani magonjwa haya yasifikie kwenye matibabu yaweze kuzuiwa na nyie viongozi wetu wa dini ni watu muhimu sana mnakutana na jamii ambayo ndiyo tunalenga elimu iwafikie kwa kiasi kikubwa,”alisema Dkt. Kilima.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Baraza la viongozi wa dini mbalimbali Tanzania, Askofu. Thomas Godda aliahidi kwa niaba ya dini zote nchini kutumia nyumba za ibada kwa ajili ya kutoa elimu ya kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza ikiwa ni pamoja kubadili mtindo wa maisha yao, kufanya mazoezi na kuzingatia lishe bora na kuongeza kuwa ili binadamu aweze kufanya ibada anahitaji kuwa na afya bora.

# TANZANIA, GLOBAL FUND KUSHIRIKIANA KUIMARISHA AFUA ZA MALARIA, TB, UKIMWI

**Na Hassan Kimweri**
**DODOMA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya na Global Fund kuendelea kushirikiana ili kuimarisha afua dhidi ya Malaria, Kifua Kikuu (TB) pamoja na UKIMWI kwa kuboresha huduma za afya na upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba.

Waziri wa afya Mhe. Jenista Mhagama alisema hayo Julai 01, 2025 alipokutana na Mkuu wa Idara ya usimamizi wa ruzuku kutoka Mfuko wa Kimataifa (Global Fund) Bw. Edwin Edington katika ofisini za wizara Jijini Dodoma.

Waziri Mhagama alisema mazungumzo hayo yamelenga kujadili masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya afya nchini kwa lengo la kutekeleza malengo ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora ya afya katika maeneo yao.

"Serikali ya Tanzania itaendelea kushirikiana na mfuko huu kwakuwa umekuwa na mchango mkubwa katika kuwezesha bidhaa za afya ikiwemo dawa, vifaa na vifaa tiba kama ilivyo azima ya Serikali ya awamu ya Sita (6) ya kujenga miundombinu na kuboresha masuala ya tiba kwa wananchi," alisema Waziri Mhagama

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya usimamizi wa Ruzuku Bw. Mark Edington kutoka Mfuko wa Kimataifa wa kusaidia mapambano dhidi ya UKIMWI, TB na Malaria (GLOBAL FUND) aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na mfuko huo katika kupiga vita maradhi ya Kifua Kikuu, Malaria na Ukimwi.

Bw. Edington aliahidi kuwa Mfuko wa Dunia utaendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za kukabiliana na magonjwa hayo hapa nchini kwa kuelekeza rasilimali fedha kwa ajili ya kununua dawa pamoja na kuboresha mifumo ya utoaji huduma ya afya.

Katika kikao hicho pia kilihudhuriwa na timu kutoka Wizara ya Afya ikiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. Seif Shekaaghe pamoja na Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Grace Magembe.






# SERIKALI YAPOKEA VIFAA VYA SHILINGI MILIONI 569.7 KWA AJILI YA HUDUMA ZA SARATANI YA MATITI

**Na Abdulwaheed Madege**
**DAR ES SALAAM**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. Seif Shekalaghe amepokea vifaa tiba kwa ajili ya huduma za saratani ya matiti vyenye thamani ya Shilingi Milioni 569.7 kutoka shirika la Jhpiego Tanzania kupitia mradi wake wa BEAT Breast Cancer.

Makabidhiano hayo yalifanyika Julai 29, 2025 katika ofisi ndogo za Wizara ya Afya jijini Dar es Salaam, ambapo Dkt. Shekalaghe alisema vifaa hivyo vitasaidia kubaini saratani ya matiti katika hatua za awali na kuanza matibabu mapema, hatua itakayosaidia kupunguza vifo vinavyotokana na ugonjwa huo.

Alieleza kuwa vifaa vilivyopokelewa ni pamoja na mashine 31 za ultrasound, sindano zaidi ya 10,000 za vipimo vya saratani ya matiti, pamoja na meza 31 za kubebea mashine hizo. Vifaa hivyo vitasambazwa katika mikoa yenye uhitaji mkubwa na idadi kubwa ya wanawake waliothirika na ugonjwa huo ikiwemo Mtwara, Morogoro na Tanga.

"Jumla ya thamani ya vifaa hivi tunavyopokea ni takribani Shilingi Milioni 569.7. Tunaamini vitakwenda kuokoa maisha ya watu wengi, hususan wanawake," alisema Dkt. Shekalaghe.

Aidha, alitoa pongezi na shukurani kwa Shirika la Jhpiego kwa kuendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania, hasa katika kipindi hiki ambacho dunia inakabiliwa na changamoto mbalimbali za kiuchumi.

Mradi wa BEAT Breast Cancer unatekelezwa kwa ufadhili wa Pfizer Foundation, kwa ushirikiano wa karibu na Wizara ya Afya pamoja na Ofisi ya Rais TAMISEMI

# SIKU YA HOMA YA INI DUNIANI

**28 JULAI, 2025**

## Dalili za ugonjwa wa homa ya ini



- Ngozi na macho kuwa na rangi ya njano
- Kukosa nguvu, kichefuchefu na kutapika
- Homa
- Tumbo kuuma upande wa juu kulia
- Kupungua uzito
- Kuumwa kichwa na mafua

*"Ondoa Vikwazo, Tokomeza Homa ya Ini"*





**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**WIZARA YA AFYA, TANZANIA, TOLEO LA MWEZI JULAI, 2025**